

UFUGAJI NYUKI UNAKIMU MAISHA SABABU 10 MUHIMU ZA KUFUGA NYUKI



Uchavushaji wa maua

1

Nyuki huchavusha maua ya mimea mbalimbali ikiwa ni kazi muhimu sana kwa maisha ya viumbe wote. Mimea ikipata huduma bora ya uchavushaji hutoa mbegu nyingi na matunda mengi yenye ubora na hufanya mimea kuongezeka na kufanya uwepo wa bioanwai.



Uendelevu

6

Ufugaji nyuki hauleti uharibifu wa Mazingira na ni shughuli endelevu. Wafugaji Nyuki ni rafiki wa mazingira asilia na wako tayari kushiriki katika uhifadhi wa misitu na mimea ambapo wanaishi na wanapopata malisho yao.



Mazao muhimu ya nyuki

2

Asali ni chakula bora chenye vitutubisho kwa afya na kinachokubalika na jamii zote na ni dawa. Nta hutumika kutengeza mishumaa na vipodozi na matumizi mengine. Chavua na gundi ya nyuki ni mazao mengine ya nyuki ambayo yanaweza kuvunwa na kutumika.



Manufaa kwa sekta mbalimbali

7

Kunapokuwa na shughuli za ufugaji nyuki, watu wengine kwenye jamii hupata fursa ya kipato kwa kutengeneza vifaa vya ufugaji nyuki, kuuza mazao ya nyuki na kutengeneza bidhaa zitokanazo mazao ya nyuki.



Matumizi ya ardhi

3

Nyuki hutembelea maua mahali popote yalipo, ya mweituni, yaliyopandwa na yaliyopo katika maeneo yaliyohifadhiwa. Maua yote yana manufaa kwa ufugaji nyuki. Ufugaji Nyuki hautumii ardhi ambayo inatumika kwa ajili ya kilimo cha mazao.



Faida linganishi

8

Katika nchi zinazoendelea ambazo kuna utajiri wa maliasili na makundi imara ya nyuki, kuna uwezekano mkubwa wa fursa ya masoko ya asali mahuluki iliyothibitishwa.



Unafuu wa gharama

4

Shughuli za ufugaji nyuki zinaweza kufanyika kwa gharama ndogo. Mizinga na vifaa vingine vyaweza kutengenezwa kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika eneo husika na nyuki ni rasilimali ya bure. Nyuki hawategemei chakula kutoka kwa mfugaji.



Pato wakati wa majanga

9

Ufugaji nyuki una manufaa wakati yanapotokea maafa. Jamii iliyokubwa na maafa huweza kujikimu mapema kwa kutengeneza mizinga na kufaidika kwa muda mfupi. Haihitaji Mfugaji Nyuki kumiliki ardhi au kuwa na makazi ya kudumu.



Vyanzo vya mapato

5

Pale mfugaji nyuki anapokuwa uhakika wa soko, ufugaji nyuki huleta faida kwa muda mfupi.



Huhusisha jinsia na rika zote

10

Ufugaji nyuki unaweza kufanywa na wanawake au wanaume wa rika zote. Nyuki hawahitaji kuhudumiwa muda wote na kazi nyingine zinaweza kufanyika sanjari na ufugaji nyuki.

Bees for development works to assist people in developing countries by providing information and advice about apiculture. **Bees for development** works worldwide, assisting beekeepers on every continent.

We acknowledge The Waterloo Foundation and Size of Wales for sponsorship of this poster.



Bees for development

1 Agincourt Street

Monmouth

NP25 3DZ, UK

+44 (0)1600 714848

info@beesfordevelopment.org

Bees for development

INFORMATION POSTER No 1 ISBN 9781898807070

www.beesfordevelopment.org

Bees for development Trust UK Registered Charity Number 1078803